

**Maombi ya Kurekebisha Bei za Umeme
Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**

Utangulizi

1. Tarehe 11 Oktoba 2013, Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO) liliwasilisha maombi ya kurekebisha bei ya umeme kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). TANESCO iliwasilisha mbele ya Mamlaka maombi manne yafuatayo:

- a) kurekebisha bei ya umeme kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 1 Oktoba 2013. Bei zirekebishwe kwa kiwango cha asilimia 67.87% kuanzia tarehe 1 Oktoba 2013, asilimia 12.74% kuanzia tarehe 1 Januari 2014 na asilimia 9.17% kuanzia tarehe 1 Januari 2015;
- b) kuidhinishwa kwa kanuni ya kurekebisha bei (indexation fomular) ya umeme kulingana na mabadiliko ya bei za mafuta na viashiria vya uchumi vinavyoathiri bei za vifaa ambazo haziwezi kudhibitiwa na TANESCO, ili kusaidia kuboresha mapato na kulifanya shirika kuwa endelevu;
- c) kuidhinishwa viwango vya bei za kuunganisha umeme vinavyozingatia ruzuku iliyotolewa na Serikali;
- d) kuidhinishwa tozo mbalimbali za huduma zilitolewazo na TANESCO.

2. Katika kuchambua maombi ya TANESCO, Mamlaka ilizingatia Sheria ya EWURA, Sura 414; Sheria ya Umeme, Sura 131; Sera ya Nishati ya mwaka 2003; na mwongozo wa uwasilishaji wa maombi ya kurekebisha bei wa EWURA wa mwaka 2009. Vifungu Na. 23(2) na 24(2) vya Sheria ya Umeme vinaitaka Mamlaka kurekebisha bei za umeme kila baada ya miaka mitatu (3) ili kuwa na bei zisizobadilika badilika katika tasnia ya umeme.

3. Kwa kuzingatia vifungu vya Sheria vilivyotajwa, na

Gharama za Huduma ya Umeme (Cost of Service Study) zilizopendekezwa na Mtaalamu Mwelekezi, AF-MERKADOS, Mamlaka imekokotoa bei ya umeme kwa kipindi cha miaka mitatu ambayo inazingatia uwepo wa huduma ya umeme endelevu hapa nchini.

Uhalali wa
Marekebisho
ya Bei

4. Kwa mujibu wa TANESCO, kupitishwa kwa maombi haya kutaliwezesha Shirika kupata fedha za kulipia gharama za uendeshaji na kuliwezesha Shirika kupata fedha za uwekezaji kwenye miundo mbinu (CIP), kulifanya Shirika liweze kukopesheka na hivyo kuwaondolea wasiwasi wahisani ambao wanatoa ruzuku na mikopo nafuu, kuliwezesha Shirika kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya umeme kwenye gridi ya Taifa (peak demand) na kuongeza uwezo wa kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya miundo mbinu iliyopo ili kuwezesha upatikanaji huduma za umeme za uhakika kwa wateja.

Ushirikishwaji
wa Wadau
wa Huduma
za Umeme

5. Kulingana na Kifungu Na. 19(2) (h) cha Sheria ya EWURA, Mamlaka ilifanya Taftishi ili kupata maoni juu ya ombi la kurekebisha bei za umeme. Taftishi ilianza tarehe 7 Novemba, 2013 na kumalizika tarehe 4 Desemba, 2013. Matangazo mbalimbali juu ya Taftishi kuhusiana na maombi ya TANESCO yalisambazwa kwenye vyombo vya habari yakiwemo magazeti na katika tovuti ya EWURA ili kupata maoni kuhusu uhalali wa maombi hayo. Ukusanyaji wa maoni ulihusisha pia mikutano minne (4) iliyofanyika Iringa na Shinyanga tarehe 15 Novemba 2013, Bagamoyo tarehe 20 Novemba na kuhitimishwa Dar es Salaam tarehe 22 Novemba 2013.

6. Katika kipindi husika, Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) lilifanya kikao chake tarehe 11 Novemba 2013 na Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) walifanya kikao chake tarehe 10 Novemba ili kutoa maoni yao juu uhalali wa maombi ya TANESCO. Hali kadhalika wananchi walipewa fursa ya kutoa maoni yao kwa maandishi na kuyawasilisha EWURA.

7. GCC walikuwa na mashaka juu ya ongezeko kubwa la asilimia 67.87% kuwa litaongeza mfumuko wa bei na gharama za maisha. Pia, GCC waliguswa na kiwango cha upotevu wa umeme kwa asilimia 24.9% ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika cha asilimia 15%. Baraza pia lilisikitishwa na

ongezeko la wizi wa umeme na ongezeko la gharama za uendeshaji zinazotokana na ununuaji wa umeme kutoka kwenye mitambo binafsi ya uzalishaji wa umeme wa dharula (EPPs).

8. Vilevile, Baraza halikuridhishwa na namna ambavyo TANESCO ilikokotoa bei kwa kutumia "Revenue Requirement" badala ya kutumia mapendekezo ya ripoti ya Gharama za Huduma ya Umeme (Cost of Service Study) ya AF-MERCADOS. Baraza lilishauri kuwa kanuni ya ukokotoaji wa bei bila usimamizi wa Mamlaka utafanya bei za umeme zisiwe za uhakika kwa watumiaji. Pia, Baraza lilishauri kuwa Shirika linatakiwa kuundwa upya ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika kutoa huduma zake.

9. EWURA CCC ilipinga upandishaji wa bei ya umeme zaidi ya ile iliyopendekezwa na Mshauri Mwelekezi, AF-MERCADOS. EWURA CCC inaona mapendekezo ya bei ya TANESCO kwa kipindi cha Oktoba 2013 mpaka Desemba 2015 ni sawa na mapendekezo ya asilimia 155% yaliyowasilishwa wakati wa kipindi cha dharula Novemba 2011. Vilevile, Baraza lilikuwa na mashaka kuwa TANESCO itaweza kuunganisha wateja 250,000 kwa mwaka 2014 kwani lengo linaloonekana kuwa kubwa mno ikilinganishwa na uwezo wa kuunganisha wateja ulioonyeshwa na TANESCO katika miaka ya nyuma. Pia iliona kwamba kutofikiwa kwa malengo ya mauzo hakukusababishwa na wateja wa migodini, bali ni bei kubwa ya umeme na kiwango cha ubora kuwa chini na usio wa uhakika.

10. Wananchi walikuwa na wasi wasi kuwa ongezeko hilo litaathiri uchumi wa nchi kwa kupuguza ushindani wa viwanda na hivyo kupelekea kupunguzwa kwa wafanyakazi viwandani. Wananchi walipendekeza kutumika kwa bei kama zilivyo pendekezwa na Mshauri Mwelekezi AF-MERCADOS. Pia, walitaka TANESCO iongeze ufanisi katika utendaji na kuboresha kiwango na uhakika wa upatikanaji umeme.

11. TANESCO ilitoa maelezo juu ya maoni yaliyotolewa na wadau kama ifuatavyo: (a) uhalali wa ombi la kurekebisha bei umetolewa katika wasilisho (Kifungu cha 1 cha Order hii). Kwamba ongezeko la bei kwa wateja wa viwandani na migodi ni kidogo ukulinganisha na gharama za kuzalisha umeme wao wenyewe. (b) kwa mwaka huu, TANESCO imevuka lengo na kuunganisha wateja 125,000 mpaka mwisho mwa mwezi

Oktoba 2013 na mpaka Desemba 2013 wengine 25,000 wanatarajiwa kuunganishwa; (c) Shirika linajitahidi kupunguza upoteaji wa umeme kwenye mifumo yake ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; na (c) Shirika linatarajia kupunguza utegemezi wa EPPs kwa kuanza kutumia mitambo ya gesi asilia kuanzia mwaka 2015.

12. Mpaka mwisho wa kipindi cha ukusanyaji wa maoni tarehe 4 Desemba 2013, Mamlaka imeridhika na maoni yaliyowasilishwa kuwa yataiwezesha kutoa maamuzi ya kina ya ombi la TANESCO.

13. Tarehe 6 Desemba 2013, EWURA iliitisha mkutano wa mwisho wa wadau wakiwemo wawakilishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini(MEM), TANESCO, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), CTI, CCC na GCC, Umoja wa wazalishaji wa saruji wa Afrika Mashariki, na ALAF. EWURA iliwasilisha muonekano wa bei na namna zilivyokokotolewa na maoni yaliyotolewa yamezingatiwa katika kutoa maamuzi ya mwisho.

14. Baada ya uchambuzi wa kina, Mamlaka imejiridhisha kuwa maombi ya kurekebisha bei na gharama mbalimbali za TANESCO ni sahihi isipokuwa vipengele vichache vilivyotajwa kwenye Aya Na. 15 mpaka 17 ambapo marekebisho madogo yamefanywa ili kuwezesha maamuzi kufanyika.

15. Mamlaka imetumia kanuni ya Ukokotoaji wa bei (Rate Setting Methodology) kama ilivyopendekezwa na AF-MERCADOS wakati wa kukokotoa mahitaji ya mapato (Revenue Requirement) ya TANESCO. Kanuni iliyopendekezwa inasaidia kutambua gharama zenye tija kwa matumizi ya sasa na baadaye na kutoa bei za gharama za miundo mbinu na nishati yenye uwiano wa mahitaji ya ongezeko la uzalishaji na usafirishaji wa umeme. Kanuni hiyo inawezesha kukokotoa bei landana na gharama (cost reflective tariffs) zinazozingatia gharama halisi kwenye mfumo wa umeme na kuzigawa kwenye makundi ya wateja kadri kila kundi linavyopata huduma, na hii ni sahihi kulingana na kifungu na. 23(2)(f) cha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008.

16. Mamlaka imerekebisha takwimu zinazoingizwa kwenye kanuni kwa lengo la kuhisha viashiria vya utendaji wa TANESCO kama ulivyo kwa mwaka 2013. Mamlaka imedurusu na kulinganisha uzalishaji (generation plan) halisi kama ulivyo kwa mwaka 2013 na kukuta kuwa kuna tofauti. Katika mwaka

Uchambuzi
na
Marekebisho
ya bei.


2013, takwimu halisi za kuanzia Januari mpaka Oktoba na makisio kwa Novemba na Desemba ilitumika. Kwa mwaka 2014 na 2015, Mamlaka ilidurusu matumizi halisi ya mitambo ya maji (hydro plants) katika kipindi kuanzia mwaka 2007 mpaka 2013 na matokeo yake yalitumika kukisia kiwango cha umeme utakaozalishwa kutoka katika mitambo ya maji. Kiasi kilichobaki cha mahitaji ya umeme kilitokana na mitambo ya mafuta (thermal plants) kwa kuanza na vyanzo vyenye gharama ndogo. Makisio mengineyo ikiwa ni pamoja na matumizi halisi ya nishati katika kuzalisha unit moja (heat rate), gharama zisizobadilika (fixed costs) na gharama zibadilikazo (variable costs) kwa kila mtambo wa kuzalishia umeme zimeachwa kama ilivyopendekezwa katika utafiti wa Gharama za Huduma (Cost of Service Study).

17. Mamlaka imechambua kanuni ya kurekebisha bei za mafuta (Fuel indexation mechanism) iliyopendekezwa na TANESCO na kuona kuwa ina mapungufu ya kiudhibiti kama vile kukosekana kwa matumizi halisi ya mitambo. Kuhusu mfumuko wa bei na mabadiliko ya Thamani ya fedha, TANESCO ilipendekeza ripoti za Benki Kuu ya Tanzania zitumike kufanya marekebisho ya bei. Kutokana na mapungufu hayo, kanuni itakayotumika ni ile iliyopitishwa na EWURA kama inavyoainishwa katika Jedwali la Kwanza (First Schedule) la kanuni Na. 7(2) ya Kanuni za Kukokotoa Bei (the Electricity (Tariff Setting) Rules) za mwaka 2013.

Ulinganishaji
wa Bei za
Umeme

18. Katika kulinganisha bei ya umeme ya Tanzania na bei za umeme katika nchi za Afrika Mashariki, imeonyesha kwamba bei mpya ya nishati (energy charge), hasa kwa matumizi ya kawaida na ya viwandani ipo chini kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki kama inavyoonyesha katika kielelezo cha 1.

Mchoro Na. 1: BEI ZA UMEME KATIKA NCHI ZA AFRIKA YA MASHARIKI



Chanzo: EWURA, ERC-Kenya, EWSA-Rwanda, ERA-Uganda.

Uamuzi

19. Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA iliyokaa tarehe 10 Desemba 2013 kufanya maamuzi juu ya maombi ya TANESCO imeamua kama ifuatavyo:-

AGIZO Na. 13-007

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na. 23(2) and 24(2))

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ("TANESCO") AGIZO LA KUREKEBISHA
BEI ZA UMEME KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU, 2013**

- Kichwa cha Agizo 1. Agizo hili litajulikana kama Shirika la Umeme Tanzania ("TANESCO") Agizo la Kurekebisha Bei ya Umeme katika Kipindi cha Miaka Mitatu, 2013.
- Kuanza kutumika 2. Agizo hili litaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Januari 2014.
- Orodha ya Bei na Tozo 3. (1). Orodha ya Bei ya huduma ya umeme na tozo mbalimbali zitakazoanza kutumika kuanzia tarehe 1 Januari 2014 zimeainishwa katika Jedwali la Kwanza na la Pili la Agizo hili. Bei zilizoidhinishwa ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 39.19 ikilinganishwa na bei ya sasa.
- (2). Bei na gharama za maunganisho kwa wateja wapya na nyinginezo zitatumika hadi tarehe 31 Disemba 2016, isipokuwa kama utafiti wa Gharama za Huduma utakaofanyika mwaka 2015 utapendekeza bei mpya..
- Mipango ya Uwekezaji 4. (1). TANESCO inatakiwa kutekeleza Miradi yake ya Uwekezaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Agizo hili, kwa kutumia fedha zitakazokusanywa kutokana na bei zilizoidhinishwa.
- (2). EWURA inaweza kurekebisha bei ya umeme ya TANESCO mwishoni mwa mwaka 2014 na/au mwaka 2015 endapo TANESCO itashindwa kutekeleza miradi iliyotajwa katika Jedwali husika. Marekebisho hayo yatatokana na makadirio ya gharama za miradi ambayo haikutekelezwa.
- Matarajio ya Vifaa vitakavyoongezwa katika mfumo wa usambazaji umeme 5. Katika kuongeza na kufanya matengenezo, katika mfumo wa kusambazia umeme, TANESCO itaongeza vifaa (Physical Units) katika mfumo wa Usambazaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.
- Gharama za mafuta, mfumuko wa bei na ubadilikaji wa thamani ya fedha 6. Kulingana na vifungu, namba 23(2) na 23(3) vya Sheria ya Umeme, Mamlaka itafanya marekebisho ya bei ya umeme ili kufidia mabadiliko ya bei za mafuta, thamani ya fedha na mfumuko wa bei. Na marekebisho haya yatafanywa kwa mujibu wa Kanuni Na. 7 ya Kanuni za Kukokotoa Bei ya umeme ya 2013.

4. TANESCO itatekeleza yafuatayo:

- (a) kuzalisha umeme kwa kutumia mitambo yenye gharama nafuu ("least cost merit order") na kuwasilisha ripoti kwa Mamlaka katika kila mwezi ikionyesha uzalishaji halisi na mpangho wa uzalishaji kama ilivyoidhinishwa na Agizo hili;
- (b) kuhakikisha kuwa zabuni za miradi ya uzalishaji umeme zinatolewa kulingana na mahitaji kama ilivyoidhinishwa kwenye Mpango wa Umeme wa Taifa (Power System Master Plan). Miradi yote mipya lazima ipatikane kwa njia ya ushindani kwa kufuata Sheria ya Umeme, "Public Private Partnership Act", Sheria ya Manunuzi na Kanuni husika;
- (c) kuwasilisha ripoti kila baada ya miezi mitatu kuhusu viashiria vya takwimu za ugavi na uhakika wa umeme (supply and reliability) katika misongo ya 11kV, 33 kV, 66 kV, 132 kV, na 220 kV kwa kila mkoa kwa ajili ya uhakiki. Takwimu husika zinatakiwa kuonyesha jumla ya masaa mteja aliyokosa umeme kwa kila "feeder", kukosekana kwa umeme kulikopangwa (planned outages), na ambao haukupangwa (unplanned outages), idadi ya matukio ya kukosa umeme katika kila "feeder", idadi ya wateja wanaohudumiwa na kila "feeder", idadi ya wateja walioathirika na katizo la umeme katika kila "feeder" na uniti za umeme zilizokosekana (total unserved energy in kWh);
- (d) kuwasilisha kwa Mamlaka, ndani ya miezi mitatu baada kuanza kwa agizo hili, mpango wa utekelezaji wa "Demand Side Management Programme" ili uidhinishwe;
- (e) kupunguza kiwango cha upotevu wa umeme

(technical and non-technical losses) katika mtandao wa usambazaji kutoka asilimia 19% ya mwaka 2012 hadi asilimia 15.1% ifikapo mwaka 2015;

- (f) kubuni mikakati ya kupambana na uunganishaji umeme usio halali na ucheleweshaji usio wa lazima katika kutoa huduma;
- (g) kuhamisha wateja walio katika kundi la D1 kwenda T1 endapo matumizi yao ya mwezi yatazidi uniti 75 kwa miezi mitatu mfululizo;
- (h) kuwasilisha kwa Mamlaka, kabla au tarehe 31 Machi, 2014, Mpango wa kuwawekea wateja wake mita za LUKU na AMR ili kupunguza wateja wanaotumia mita za zamani (conventional meters);
- (i) kuwasilisha kwa Mamlaka, kila baada ya miezi mitatu, taarifa/ripoti ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake ili kuongeza mapato ya shirika;
- (j) kufanya juhudi za makusudi kueneza na kuelimisha wateja wake Mkataba wa Huduma kwa Wateja na kuhakikisha daima inashughulikia kero za wateja kama inavyoelekezwa katika Mkataba husika na Kanuni;
- (k) kuwasilisha kwa Mamlaka, maombi ya ya marekebisho ya bei yatoakanayo na mabadiliko ya bei za mafuta, mfumuko wa bei na ubadilikaji wa thamani ya fedha; Ukokotoaji wa marekebisho hayo utakuwa kama ulivyoainishwa katika Kanuni ya 7 ya Kanuni za Kupanga Bei za Umeme za mwaka 2013 (Electricity (Tariff Setting) Rules, 2013);
- (l) kuendelea kutoa taarifa kwa Mamlaka kuhusu hali ya kifedha na kiundeshaji kama inavyotakiwa. Taarifa hizi

zitatumiwa na Mamlaka katika kutathmini utendaji wa TANESCO ikilinganishwa na mashirika mengine ya umeme katika nchi jirani ili kuboresha utendaji wake. Tathmini hii pia itatumiwa na Mamlaka katika kubaini uhalali wa maombi ya baadae ya kurekebisha bei;

(m) kuwasilisha kwa Mamlaka, kabla au tarehe 31 Machi 2014, mpango wa utekelezaji wa kila Sharti la Agizo hili.

Kufutwa kwa Agizo

5. Agizo hili linafuta Agizo Na. 001-013 la tarehe 24 Januari 2013 la Shirika la Umeme Tanzania ("TANESCO") linalohusu Marekebisho ya Bei za Umeme.

JEDWALI LA KWANZA: BEI YA UMEME ILIYOIDHINISHWA

Kundi la Mteja	Aina ya Bei	Uniti	Bei zinazotumika sasa	Bei zilizoidhinishwa			Ongezeko (TZS)
				2013	2014	2015	2014
D-1	Tozo la kutoa Huduma	TZS/mwezi	-	-	-	-	
	Bei ya Nishati(Uniti 0 - 75)	TZS/uniti	60	100	100	100	40
	Zaidi ya Uniti 75	TZS/uniti	273	350	350	350	
							0
T-1	Tozo la kutoa huduma	TZS/mwezi	3,841	5,520	5,520	5,520	1,679
	Bei ya Nishati	TZS/uniti	221	306	306	306	85
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/mwezi		-	-	-	-
							0
T-2	Tozo la kutoa huduma	TZS/mwezi	14,233	14,233	14,233	14,233	0
	Bei ya Nishati	TZS/uniti	132	205	205	205	73
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/mwezi	16,944	15,004	15,004	15,004	-1,940
T-3_MV	Tozo la kutoa huduma	TZS/mwezi	14,233	16,769	16,769	16,769	2,536
	Bei ya Nishati	TZS/uniti	118	163	163	163	45
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/mwezi	14,520	13,200	13,200	13,200	-1,320
T-3_HV	Tozo la kutoa huduma	TZS/mwezi	14,233	-	-	-	-
	Bei ya Nishati	TZS/uniti	106	159	159	159	53
	Bei ya Mahitaji ya Juu	TZS/kVA/uniti	12,079	16,550	16,550	16,550	4,471
Key							
<p>D1: Wateja wa majumbani ambao wana matumizi madogo ya wastani wa uniti 75 kwa mwezi. Matumizi yakizidi uniti 75 yatatozwa bei ya juu ya shilingi 350 kwa uniti moja. Under this category, power is supplied at a low voltage, single phase (230 V).</p>							
<p>T1: Wateja wenye matumizi ya jumla ya umeme hususani watumiaji wakubwa wa majumbani, matumizi ya biashara ndogondogo, viwanda vidogovidogo, taa za barabarani, mabango, n.k. Umeme unatolewa katika msongo volteji ndogo kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V).</p>							
<p>T2: Wateja wenye matumizi ya kawaida ambapo hupimwa kwa volti 400 na matumizi ya wastani ni zaidi ya uniti 7,500 kwa mwezi.</p>							
<p>T3_MV: Wateja waliunganishwa katika msongo wa uneme wa kati (Medium Voltage).</p>							
<p>T3_HV: Wateja wakubwa ambao wameunganishwa katika msongo wa juu (High Voltage) ikiwa ni pamoja na ZECO, Bulyanhulu, Twiga Cement.</p>							

JEDWALI LA PILI: GHARAMA ZA KUUNGANISHA WATEJA WAPYA

Na. 1: Gharama katika Mfumo wa Njia Moja ya Umeme (Single Phase Charges)

Njia ya Umeme	Gharama Husika TZS (pasipo VAT)	Bei ya Kuunganisha iliyopendekezwa (TZS)			Bei ya Kuunganisha iliyoidhinishwa (TZS)		
		Bei yenye Ruzuku kwa MijiniTZS (bilaVAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Mijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Lindi na Mtwara TZS (VAT ikiwemo)	Bei yenye Ruzuku kwa Mijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Lindi na Mtwara (itatumika hadi 30 Juni 2014 tu) TZS (VAT ikiwemo)
Ndani ya Meta 30	385,682	272,000	150,000	99,000	272,000	150,000	99,000
Umbali usiozidi Meta 70 (nguzo moja)	1,145,664	436,964	286,220	N/A	436,964	286,220	N/A
Umbali usiozidi Meta 120 (nguzo mbili)	1,696,120	590,398	385,300	N/A	590,398	385,300	N/A
Ada ya Maombi	5,000	5,000	5,000	5,000	5,000	5,000	5,000

Angalizo: VAT ni Kodi ya Ongezeko la Thamani

Na. 2: Gharama katika Mfumo wa Njia Tatu za Umeme (Three Phase Charges) kwa Wateja wa Mijini na Vijijini

Njia ya Umeme	Aina ya Mita (Dira)	Gharama Husika TZS (pasipo VAT)	Bei ya kuunganisha iliycopendekezwa (TZS)			Bei ya Kuunganisha iliyoidhinishwa (TZS)		
			Bei yenye Ruzuku kwa Mijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Lindi na Mtwara TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Mijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Vijijini TZS (pasipo VAT)	Bei yenye Ruzuku kwa Lindi na Mtwara (Itatumika hadi 30 Juni 2013) TZS (pasipo VAT)
Umbali usiozidi Meta 30 (waya (cable) 16mm ²)	LUKU	772,893	772,893	772,893	99,000	772,893	772,893	99,000
Umbali usiozidi Meta 30 (waya (cable) 16mm ²)	AMR	880,772						
Umbali usiozidi Meta 30 (waya (cable) 35mm ²)	LUKU	913,202						
Umbali usiozidi Meta 30 (waya (cable) 35mm ²)	AMR	1,028,850						
Umbali usiozidi Meta 70 (nguzo moja)	LUKU	1,799,062	1,058,801	1,058,801	N/A	1,058,801	1,058,801	N/A
Umbali usiozidi Meta 70 (nguzo moja)	AMR	1,906,939						
Umbali usiozidi Metal20 (nguzo mbili)	LUKU	2,604,391	1,389,115	1,389,115	N/A	1,389,115	1,389,115	N/A
Umbali usiozidi Metal20 (nguzo	AMR	2,712,271						

mbili)								
Ada ya Maombi		5,000	5,000	5,000	5,000	5,000	5,000	5,000

Angalizo: Bei za kuunganisha wateja wapya zenye ruzuku ya Serikali kwa mikoa ya Lindi and Mtwara (kwa mifumo ya njia moja na njia tatu za umeme) zitakoma tarehe 30 Juni 2014. Kuanzia tarehe 1 Julai 2014, gharama za kuunganisha wateja katika mikoa hiyo miwili zitakuwa kama zilivyoidhinishwa kwa Wateja wa Mijini na Vijijini.

Na. 3: Gharama za kufunga mita zilizo haribika au kuchezewa na wateja

Kundi la Mteja	Maelezo	Bei iliyopendekezwa pasipo VAT	Bei iliyoidhinishwa pasipo VAT)
D1& T1	LUKU (Njia moja)	60,000	60,000
	LUKU (Njia Tatu)	200,000	200,000
	AMR (Njia Tatu)	300,000	300,000
T2	Mita zinazotumia CT	1,200,000	1,200,000
T3	Mita zinazotumia CT/VT	1,200,000	1,200,000

Na. 4: Gharama za Majaribio ya Mita (Meter Testing Fees)

Kundi la Mteja	Bei ya zinazotumika sasa (pasipo KVAT)	Bei iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Bei iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1	3,000	5,000	0
T1	3,000	5,000	0
T2	30,000	50,000	0
T3	50,000	100,000	0

Na. 5: Gharama za kujaribu na kukaguwa Ufungaji (Testing and Inspection of Installation Charges)

Kundi la Mteja	Bei iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Bei iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1	20,000	20,000
T1	20,000	20,000
T2	30,000	30,000
T3	50,000	50,000

Na. 6: Gharama za Uunganishaji Umeme wa Muda Mfupi (Temporary Power Supply Charges)

Kundi la Mteja	Maelezo	Bei iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Bei iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
T2	Ada ya Maombi	5,000	5,000
T3		5,000	5,000
T2	Gharama za Kuunganishwa	Malipo Halisi na 10%	Malipo Halisi na 10%
T3		Malipo Halisi na 10%	Malipo Halisi na 10%
T2	Malipo ya Amana ya Mita (Meter Deposit)	200,000	200,000
T3		500,000	500,000

Jedwali Na. 7: Malipo ya Amana ya Umeme (Energy Deposit for Post-paid Meters)

Kundi la Mteja	Maelezo	Bei iliyopendekezwa (pasipo VAT)	Bei iliyoidhinishwa (pasipo VAT)
D1	Njia Moja	30,000	30,000
T1	Njia Moja	30,000	30,000
T1	Njia Tatu	150,000	150,000
T2	Njia Tatu	200,000	200,000
T3	Njia Tatu	500,000	500,000

Gharama ya Urejeshaji Umeme ni TZS 7,000 (pasipo VAT).

Tozo la kuchezeza Mita za TANESCO (Metering System) kwa Wateja wa D1, T1, T2 na T3 itakuwa kama inavyoelekezwa katika Kanuni mpya za Huduma za Ugavi wa Umeme za mwaka 2013.

**JEDWALI LA TATU: MIRADI ILIYOIDHINISHWA ILI KUTEKELEZWA KWA
GHARAMA ZA UWEKEZAJI (CAPITAL INVESTMENT PROJECTS) TANESCO
MIAKA YA 2014 NA 2015**

Makisio ya gharama zilizopitishwa kama zilivyoombwa na TANESCO zitakuwa TZS 908.4 billion katika mwaka wa 2014 na TZS 449.0 bilioni kwa mwaka 2015 kama zinavyoonyeshwa kwenye Jedwali 1, 2 na 3 hapa chini :

Na.1: Miradi ya Usafirishaji Umeme

Miradi ya Usafirishaji Umeme	2014	2015	Total
	TZS 'm	TZS 'm	TZS 'm
Makambako – Songea (220kV)	12,000	--	12,000
Kuboresha Njia ya Kusafirisha Umeme ya Kipawa (132kV) Njia ya Pili	109	--	109
Kupanua wigo wa Fibre Optic Network	1,103	--	1,103
Hydro-Thermal "Scheduling and Optimisation"	--	8,000	8,000
Vifaa na Vitendea kazi mbalimbali	1,203	400	1,603
Karakana Mpya ya Umeme	779	--	779
Kubadilisha "Control" na "Switchgear Protection"	13,585	4,000	17,585
Fidia za Mradi wa Usafirishaji umeme (Backbone Project)	5,339	--	5,339
Genereta ya umeme kwa ajili ya "Control Centres"	228	--	228
Geita - Nyakanazi (220kV)	16	--	16
Ukarabati wa njia ya usafirishaji umeme kutoka Ubungo –Chalinze – Hale (132kV)	4,080	2,040	6,120
Miradi mingineyo	1,373	200	1,573
Jumla ya Gharama	39,814	14,640	54,454

Na. 2: Miradi ya Usambazaji Umeme

Miradi ya Usambazaji wa Umeme	2014	2015	Total
	TZS 'm	TZS 'm	TZS 'm
Miradi mipya ya kuunganisha wateja 100,000	479,320	264,574	743,894
Ghara za kuunganisha mteja (ndani ya mita 30) kwa wateja 150,000	161,512	80,756	242,268

Miradi ya Usambazaji Umeme inayoendelea	107,019	52,497	159,515
Usambazaji wa umeme katika kijiji cha Ukami	250	--	250
Usambazaji wa umeme katika vijiji vya Magindu, Mbweze, Mgwashi and Kiwanga	25	--	25
Jumla ya Gharama	748,126	397,827	1,145,953

Na. 3: Miradi Mingineyo

Miradi Mingineyo	2014	2015	Total
	TZS 'm	TZS 'm	TZS 'm
Magari	17,305	10,500	27,805
Miradi mingine ya "Corporate Services"	34,426	13,092	47,518
Ukarabati na uboreshaji wa Mitambo ya kufua umeme ya Maji (Hydro Plants)	36,337	12,933	49,271
Fidia kwa njia ya umeme wa Mtwara (300MW Project)	25,355	--	25,355
Vifaa na vitendea kazi kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme ya mafuta na gesi asilia	4,000	--	4,000
Miradi ya REA	2,500	--	2,500
LKHP "Environmental Management"	350	--	350
Miradi ya Ufuaji Umeme kwa Upepo	193	--	193
Jumla ya Gharama	120,466	36,525	156,992

JEDWALI LA NNE:

**VIFAA (PLANNED PHYSICAL UNITS) VILIVYOPITISHWA KUONGEZWA
KATIKA MFUMO WA USAMBAZAJI UMEME (DISTRIBUTION NETWORK)
KUANZIA 2013 – 2015**

<i>(Vifaa/vitu Mbalimbali)</i>	Uniti	2013	2014	2015
Transfoma ya MV/LV - Mijini	Idadi	1,103	1,661	2,650
Transfoma ya MV/LV - rural	Idadi	2,355	3,047	4,449
Transfoma ya MVA MV/LV - Vijijini	MVA	213	321	512
Transfoma ya MVA MV/LV - Vijijini	MVA	118	152	222
Njia ya Usambazaji (MV Distribution) – Mijini	Km	2,075	3,107	4,957
Njia ya Usambazaji (MV Distribution) – Vijijini	Km	6,545	8,469	12,365
Njia ya Usambazaji (MV Distribution) – Mijini	Km	4,150	4,150	4,177
Njia ya Usambazaji (LV Distribution) – Vijijini	Km	3,625	3,625	3,625
Transfoma mpya katika 'substation (MV/MV) ya zamani	Idadi	1	1	6
"substation" mpya (MV/MV substations)	Idadi	7	7	11

Dar es Salaam

...10th Desemba, 2013



HARUNA MASEBU

Mkurugenzi Mkuu